ISSN 1866-5866 OKTOBA - DESEMBA, 2025

THE VOICE OF

# Haki

JARIDA LA TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

# DKT. MWINYI AIPONGEZA THBUB



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi*




*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (katikati) akiwa na Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Zainabu Katimba (wa Pili Kulia), Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Mhe. Jaji Mathew Mwaimu (Mst) (wa Pili kushoto), Makamu Mwenyekiti THBUB Mhe. Mohamed Khamis Hamad ( wa kwanza Kushoto), Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Dkt. Franklin Rwezimula pamoja na Manejimenti ya THBUB mara baada ya kuwasili katika Ofisi za Taasisi hiyo Novemba 26, 2025.*

**NDANI** Viongozi wa THBUB washiriki kwa vitendo Uchaguzi Mkuu 2025

# NENO LA **UTANGULIZI**

**Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) ni idara huru ya Serikali, iliyoanzishwa kama Taasisi ya kitaifa iliyo kitovu cha kukuza na kulinda Haki za Binadamu na misingi ya Utawala Bora nchini Tanzania.**

**THBUB ilianzishwa chini ya Ibara ya 129(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 3 ya mwaka 2000.**

**THBUB imepewa jukumu la kupokea na kuchunguza malalamiko ya uvunjifu wa haki za binadamu, kufanya ufafiti, ufuatiliaji wa masuala ya haki za binadamu na utawala bora sambamba na kutoa elimu.**



**Mhe. Mathew P. M. Mwaimu (Jaji Mst)**
Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

**Uanzishwaji wa jarida la Voice of Haki umelenga kutoa taarifa ya kazi mbalimbali zinazofanywa na THBUB ili kuweka uelewa kwa jamii kuhusu majukumu ya Tume na namna majukumu hayo yanavyotekelezwa katika kulinda na kukuza haki za binadamu na misingi ya utawala bora.**

**Hivyo, nichukue fursa hii kuwakaribisha kusoma jarida la robo ya kwanza kwa mwaka 2025/2026 ili kuweza kuifahamu THBUB pamoja na majukumu yake.**


**KAMATI YA UHARIRI**
**Mwenyekiti:** Monica Mnanka
**Mhariri:** Zawadi A. Msalla
**Mhariri Msaidizi:** Nuru Mfaume
**Wajumbe:** Mwashamba Juma, Tumaini Obel, Farida Ruben



**MAWASILIANO**
Mtaa wa Nyerere,
Plot Na. 339/Kilimani
S.L.P 1049 DODOMA,
Tanzania
Simu: +255 738 279744
Barua Pepe:
www.chragg.go.tz


## YALIYOMO


| | |
|---|---|
| DKT. MWINYI AIPONGEZA THBUB | UK. 3 |
| VIONGOZI WA THBUB WASHIRIKI KUPIGA KURA KATIKA UCHAGUZI MKUU 2025 | UK. 4 |
| DKT. JUMA HOMERA: THBUB NI NGUZO MUHIMU YA ULINZI WA AMANI YA TAIFA | UK. 5 |
| THBUB YAANZA UCHUNGUZI WA MATUKIO YA UVUNJIFU WA HAKI ZA BINADAMU WAKATI WA VURUGU KIPINDI CHA UCHAGUZIMKUU | UK. 6 |
| THBUB YASHIRIKIANA NA WADAU KULINDA HAKI ZA WAVUVI WADOGO | UK. 7 |
| THBUB YAIMARISHA UZINGATIAJI WA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA DAR ES SALAAM | UK. 8 |
| THBUB YAWAJENGEA UWEZO MADIWANI WA HALMASHAURI ZA JIJI LA DAR ES SALAAM | UK. 9 |
| HABARI PICHA | UK. 10-11 |
| HABARI PICHA | UK. 12-13 |



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu Zanzibar yaliyofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Dimani, Mkoa wa Mjini Magharibi, Dis¬emba 15, 2025.*

# DKT. MWINYI AIPONGEZA THBUB

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, ameipongeza Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa kuendelea kushughulikia malalamiko ya wananchi kuhusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Dkt. Mwinyi ametoa pongezi hizo katika kilele cha maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu yaliyofanyika viwanja vya maonesho ya biashara Nyamazi, Wilaya ya Magharibi B, Mkoa wa Mjini Magharibi, Disemba 15, 2025.

Amesema Tanzania imeendelea kupiga hatua kubwa katika utekelezaji wa Malengo ya Umoja wa Mataifa yanayohusiana na haki za binadamu na mapambano dhidi ya rushwa kupitia uridhiaji na utekelezaji wa mikataba na mikakati ya kimataifa.

Dkt. Mwinyi pia ameipongeza THBUB jinsi inavyoendelea kushirikiana na taasisi mbal-imbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Taasisi binafsi na Asasi za Kiraia katika kufanya uchechemuzi, kulinda na kutetea haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa kuwa ushirikiano huo umesaidia ku¬kamilika na kutekelezwa kwa majukumu mbalimbali ya THBUB.

Katika kipindi cha Januari mpaka Disemba 2025, THBUB imefanikiwa kushughulikia jumla ya malalamiko thelathini na tatu (33), kati ya hayo ishirini na sita (26) yanahusu haki za binadamu na saba (7) yanahusu ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Aidha, THBUB imepokea malalamiko nane (8) kati ya yaliyopokelewa uchunguzi wake umekamilika kwa mafanikio makubwa na mengine walalamikaji wake walipewa ushauri wa kisheria na kuelekezwa kuwasilisha malalamiko yao katika mamlaka mbalimbali zinazohusika na malalamiko hayo.

Maadhimisho ya siku ya Maadili na Haki za Binadamu Duniani huadhimisha Disemba 10 ya kila mwaka ambapo kwa upande wa Zanzibar yanakua maadhimisho ya tisa kufanyika.

# VIONGOZI WA THBUB WASHIRIKI KUPIGA KURA KATIKA UCHAGUZI MKUU 2025



Katika kuzingatia misingi ya demokrasia, Haki za binadamu na Utawala bora, viongozi wa juu wa Tume ya Haki za Bin-adamu na Utawala Bora (THBUB) wamejitokeza kushiriki kikamilifu zoezi la kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani Oktoba 29, 2025.

Mwenyekiti wa THBUB, Mhe. Mathew P. M. Mwaimu (Jaji Mst), alishiriki zoezi la kupiga kura katika kituo cha Malindi Estate kilichopo Mbweni Jijini Dar es salaam. Aki-zungumza baada ya zoezi hilo Mhe. Mwaimu amesema ujenzi wa demokrasia imara unaanza na uwajibikaji wa kila mmoja, hususani viongozi wa umma na kutoa wito kwa Watanzania kujitokeze kwa wingi kumchagua viongozi wanaowataka.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa THBUB, Mhe. Mohammed Khamis Hamad, alishiriki zoezi hilo katika kituo cha kupigia kura cha Skuli ya Sekondari ya Kisauni, kilichopo Jimbo la Dimani, Shehia ya Kisauni, Wilaya ya Magharibi B, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja. Mhe. Mohammed alieleza kuwa anajivunia kuwa Mtanzania na namna nchi yake inavyozingatia misingi ya utawala bora.

Aidha, Makamishina Mhe. Thomas Masanja, Mhe. Amina Ali, Mhe. KhaMwinyichande na Mhe. Nyanda Shuli pamoja na Katibu Mtendaji, Bw.Patience Ntwina walishiriki zoezi la kupiga kura wakati wa Uchaguzi Mkuu 2025.

Ushiriki wa viongozi wa THBUB katika kupiga kura unaakisi kwa vitendo dhamira ya THBUB katika kusimamia na kuhimiza uzingatiaji wa haki za binadamu, utawala wa sheria na misingi ya uwajibikaji wa kidemokrasia.
Kwa ujumla, Uchaguzi Mkuu umeendelea kuwa jukwaa la kuimarisha demokrasia

# DKT. JUMA HOMERA: THBUB NI NGUZO MUHIMU YA ULINZI WA AMANI YA TAIFA




***Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Katikati waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Wizara ya Katiba na Sheria na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora alipotembelea katika Ofisi za THBUB Novemba 26, 2025.***

Wito umetolewa kwa jamii kuilinda na kuitunza amani ya Taifa ili iendelee kuwa alama ya pekee inayoitofautisha Tanzania na mataifa mengine duniani. Hayo yameelezwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Juma Homera, wakati wa ziara yake ya kikazi katika Ofisi za Makao Makuu ya THBUB Jijini Dodoma, Novemba 26, 2025.

Mhe. Homera alieleza kuwa amani ya Tanzania ni hazina iliyojengwa kwa miaka mingi na kuendelea kulindwa na taasisi mbalimbali za kikatiba. Miongoni mwa taasisi hizo aliitaja THBUB na kuwataka viongozi kuchukua nafasi yao kikamilifu ili kuhakikisha taasisi hiyo inaendelea kuwa chachu ya ulinzi wa amani nchini.

Ziara hiyo pia ilikuwa ni moja ya fursa ya kutathmini utekelezaji wa majukumu ya tume pamoja na kuimarisha ushirikiano kati ya Wizara na taasisi zake.

Akizungumza na viongozi na watumishi wa THBUB, Dkt. Homera amesisitiza kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeipatia Tume mamlaka makubwa ya kulinda na kuendeleza Haki za binadamu na misingi ya Utawala Bora, jambo lin¬aloenda sambamba na kudumisha amani na mshikamano wa Taifa.

“Tumekuwa kimbilio la wengi kwa sababu ya amani tuliyonayo. Amani hii ni tunda la kujivunia. THBUB mna wajibu mkubwa wa kuwaelimisha wananchi kuhusu haki zao, wajibu wao na umuhimu wa kuilinda amani iliyopo,” amesema Dkt. Homera.

Kwa mujibu wa Waziri huyo, haki za binadamu haziwezi kutenganishwa na dhana ya amani, kwani jamii inayozitambua haki na wajibu wake hujenga misingi imara ya utawala bora na mshikamano wa kitaifa. Ameeleza kuwa mchango wa THBUB hauishii katika kushughulikia malalamiko pekee, bali pia katika kutoa elimu kwa umma ili kuzuia migogoro kabla haijatokea.

Katika hatua nyingine, Dkt. Homera ameipongeza THBUB kwa weledi na uwajibikaji unaoonekana katika utekelezaji wa majukumu yake, huku akiahidi kuwa Wizara ya Katiba na Sheria itaendelea kushirikiana kwa karibu na tume hiyo kwa maslahi mapana ya Taifa.

Awali, akitoa neno la kumkaribisha Waziri, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Zainabu Katimba, amesisitiza umuhimu wa wananchi kuelewa kuwa haki na wajibu ni dhana mbili zisizotenganishwa. Ameeleza kuwa ingawa haki za binadamu zina wigo mpana, zinatekelezwa ndani ya mipaka inayoolinda haki za wengine na maslahi ya Taifa kwa ujumla.

“Kila mtu anapofurahia haki zake za msingi, ana wajibu wa kuhakikisha hafanyi hivyo kwa kuvunja haki za wengine,” amesema Mhe. Katimba.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa THBUB, Mhe. Jaji Mathew Mwaimu (Mst), akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Tume, ameishukuru Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano endelevu unaoiwezesha THBUB kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Pia, ameahidi kuwa tume itaendelea kushirikiana na Serikali katika kuimarisha ulinzi wa haki za binadamu, utawala bora na amani ya nchi.




*Mwenyekiti Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Mhe. Mathew P. M.Mwaimu (Jaji Mst.) akitoa taarifa kwa Vyombo vya Habari kuhusu kufanya Uchunguzi wa matukio ya uvunjwaji wa haki za binadamu wakati wa maandamano ya Uchaguzi Octoba 29, 2025. Mkutano huo ulifanyika katika ofisi za THBUB makao Makuu, Mtaa wa kilimani Jijini Dodoma Novemba 5, 2025.*

# THBUB YAANZA UCHUNGUZI WA MATUKIO YA UVUNJIFU WA HAKI ZA BINADAMU WAKATI WA VURUGU KIPINDI CHA UCHAGUZI MKUU

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) inatarajia kuanza uchunguzi wa kina kuhusu madai ya uvunjifu wa haki za binadamu wakati wa maandamano yaliyofanyika kipindi cha Uchaguzi Mkuu wa Rais, Ubunge na Udiwani uliofanyika Oktoba 29, 2025.

Uamuzi huo umetangazwa na Mwenyekiti wa THBUB, Mheshimiwa Mathew P. M. Mwaimu (Jaji Mst), alipokuwa akizungumza na waandi¬shi wa habari katika Ofisi za Makao Makuu ya THBUB zilizopo Mtaa wa Kilimani, Jijini Dodoma, Novemba 5, 2025. Mhe. Mwaimu amesema kuwa, THBUB inalaani vikali vitendo vyote vilivyosababisha kuvunjwa kwa haki za binadamu, ikiwemo haki ya kuishi, pamoja na matukio ya unyang'anyi na uharibifu wa mali za umma na binafsi. Alisisitiza kuwa maandamano, pamoja na kuwa ni haki ya kikatiba, hayapaswi kutumika kama kisingizio cha kukiuka sheria na haki za watu wengine.

Akizungumza kuhusu mwelekeo wa uchunguzi huo, Mheshimiwa Mwaimu alisema kuwa baada ya kukamilika, Tume itatoa mapendekezo kwa Serikali pamoja na wadau wengine ili kuimarisha ulinzi wa haki za binadamu, hususani katika vipindi vya uchaguzi. Aidha, alitumia fursa hiyo kuwakumbusha wananchi umuhimu wa kudumisha amani na utulivu kwa maslahi mapana ya Taifa. Uchunguzi huo unatarajiwa kuanza rasmi hivi karibuni, ambapo taarifa ya awali itatolewa ndani ya kipindi cha mwezi mmoja na nusu tangu kuanza kwake. Taarifa hiyo itatoa mwelekeo wa awali kuhusu matokeo ya uchunguzi pamoja na hatua zinazopendekezwa kuchukuliwa.

Hatua ya THBUB kuanza uchunguzi huo ni sehemu ya juhudi za kuimarisha utawala bora, uwajibikaji na kuheshimu haki za bi-nadamu nchini, hasa katika nyakati nyeti za mchakato wa kidemokrasia kama chaguzi.



*Katibu Mtendaji Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Bw. Patience Ntwina akifungua kikao cha kuwasilisha na kujadili rasimu ya taarifa ya uchambuzi wa awali kuhusu haki za wavuvi wadogo katika upatikanaji na usimamizi na rasilimali za Bahari, kilichofanyika Disemba 19,2025 Jijini Dodoma.*

# THBUB YASHIRIKIANA NA WADAU KULINDA HAKI ZA WAVUVI WADOGO

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) im¬eendelea kuimarisha juhudi zake za kulinda na kusimamia haki za wavuvi wadogo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika sekta ya uvuvi na uhifadhi wa mazingira ya bahari.

Hatua hiyo imebainishwa wakati wa kikao cha kuwasilisha na kujadili rasimu ya taarifa ya uchambuzi wa awali kuhusu haki za wavuvi wadogo katika upatikanaji na usimamizi wa rasilimali za bahari, kilichofanyika Jijini Dodoma Disemba 19, 2025 kwa lengo la kupata maoni na mapendekezo ku¬toka kwa wadau.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa kikao hicho, Katibu Mtendaji wa THBUB, Bw. Patience Ntwina, amesema kuwa Tume imejipanga kuhakikisha haki za binadamu zinaheshimiwa, zinalindwa na kutekelezwa kwa usawa, hususan kwa makundi yenye changamoto, ikiwemo wavuvi wadogo.

Bw. Ntwina amesisitiza kuwa wavuvi wadogo ni nguzo muhimu katika uchumi wa taifa, ustawi wa jamii za pwani na uhifadhi wa mazingira ya bahari, hivyo wanastahili kulindwa na kuwezeshwa ili waweze kunufaika ipasavyo na rasilimali zilizopo. "Kupitia ushirikishwaji wa wadau, tunahakikisha kuwa sauti za wavuvi wadogo zinasikika na kuzingatiwa katika maamuzi yanayohusu maisha yao," alisema Bw. Ntwina.

Aidha, alibainisha kuwa matokeo ya uchambuzi huo yatatoa msingi wa kuishauri Serikali na wadau wengine kuhusu maboresho ya sera, sheria, miongozo na taratibu za usimamizi wa rasilimali za bahari. Kwa upande wao, wadau walioshiriki kikao hicho, wameeleza kuwa hatua ya THBUB kuendelea kuimarisha ulinzi wa haki za wavuvi wadogo ni muhimu katika kutatua changamoto zinazowakabili wavuvi wadogo, zikiwemo upatikanaji wa maeneo ya uvuvi, masoko, mikopo, pamoja na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi.

THBUB imeahidi kuendelea kushirikiana na wadau wote husika ili kuhakikisha mapendekezo yaliyotolewa yanazingatiwa na kutekelezwa kwa vitendo kwa manufaa ya wavuvi wadogo, jamii za pwani na taifa kwa ujumla. Kupitia juhudi hizi, Tume inaamini kuwa usimamizi bora wa rasilimali za bahari utawezesha kuwepo kwa maendeleo endelevu, kulinda haki za binadamu na kuhakikisha ustawi wa kizazi cha sasa na kijacho.



*Afisa Uchunguzi Mkuu wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Bi. Neema Kafanabo akitoa mafunzo maalum kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa Chuo cha Teknolojia Dar es salaam (DIT), Novemba 25, 2025.*

# THBUB YAIMARISHA UZINGATIAJI WA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA DAR ES SALAAM

Zaidi ya wanachuo 4000 wa mwaka wa kwanza na watumishi 121 kutoka katika vyuo mbalimbali vikuu na vya kati Jijini Dar es Salaam wamepatiwa elimu ya haki za binadamu na misingi ya utawala bora kati ya Novemba 20 hadi 25, 2025. Elimu hiyo ililenga katika kujenga kizazi cha vijana kinachozingatia masuala ya haki za bindamu, wanapokuwa katika masomo yao na kuwa mabalozi na walinzi wa haki hizo katika jamii.

Wanufaika wa elimu hiyo ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Ki-kuu cha Ardhi, Chuo Kikuu kishiriki cha elimu (DUCE), Chuo cha Biashara (CBE), Chuo cha teknolojia Da es Salaam (DIT) na Chuo cha Usafirishaji (NIT).

Akizungumza na wanavyuo hao, Afisa Uchunguzi Mkuu,
Bi. Neema Kafanabo amesema hatua ya (THBUB) kutoa elimu hiyo kwa wanafunzi ni utekelezaji wa jukumu lake la Kikatiba la kukuza na kulinda haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa kuhakikisha elimu hiyo inamfikia kila mtanzania.

Pia, Bi. Neema amesema kuwa kupitia elimu hiyo washiriki wanapata fursa ya kubadilishana uzoefu wa mambo mbal-imbali yanayohusu haki za binadamu, wajibu wa raia na umuhimu wa kuheshimu haki za wengine katika jamii.
“Mafunzo haya yanalenga kuwawezesha wanachuo kuwa walinzi wa haki zao na za wengine, na kuwa nguzo ya kuimarisha utawala bora sasa na wakati ujao,”
amesema Bi. Neema.

# THBUB YAWAJENGEA UWEZO MADIWANI WA HALMASHAURI ZA JIJI LA DAR ES SALAAM



*Afisa Uchunguzi Mkuu wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Bw. Brighton Mwiga akitoa mafunzo maalum kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora kwa Madiwani wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo yaliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Manispaa hiyo Jijini Dar es salaam, Desemba 4, 2025.*

Katika juhudi za kuimarisha uongozi unaozingatia misingi ya utawala bora nchini, Tume ya Haki za Bi¬nadamu na Utawala Bora (THBUB), imeendesha mafunzo kwa madiwani wa Halmashauri za Ubungo, Kigamboni na Temeke Jijini Dar es salaam yaliyofanyika kuanzia Disemba 4 hadi 10, 2025 yakihusisha jumla ya madiwani sitini (60).

Mafunzo hayo yalilenga kuwakumbusha viongozi hao umuhimu wa kuzingatia uadilifu, uwazi, na uwajibikaji katika kusimamia rasilimali za umma na kutoa huduma bora kwa wa¬nanchi. Aidha, yaliweka mkazo umuhimu wa viongozi hao kushirikisha wananchi katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Afisa Uchunguzi Mkuu wa THBUB, Bw. Brighton Mwiga, aliwataka madiwani kutumia madaraka yao kwa kuzingatia haki za binadamu na misingi ya haki ya utawala bora.

“Uongozi bora hujengwa juu ya utawala wa sheria, uwazi, ufanisi na tija, ushirikishwaji, usawa, uadilifu, mwitiko na maridhiano” amesema Bw. Mwiga. Kupitia mafunzo hayo, washiriki walipata fursa ya kujadili changamoto mbalimbali zinazowakabili katika utekelezaji wa majukumu yao, pamoja na kubadilishana uzoefu kuhusu mbinu bora za kuimarisha uwajibikaji na uwazi katika utawala wa Serikali za mitaa. Kwa upande wao, baadhi ya madiwani walioshiriki walieleza kufurahishwa na mafunzo hayo, wakisema yamewapa mwanga mpya katika kutekeleza majukumu yao kwa weledi, uaminifu na kujituma.

# HABARI **PICHA**

## **Uchaguzi Mkuu** 2025



***Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Mhe. Mathew P. M. Mwaimu (Jaji mst), akipiga kura katika kituo cha kupigia kura cha Malindi Estate kilichopo Mbweni Jijini Dar es salaam, Oktoba 29, 2025.***

## **Uchaguzi Mkuu** 2025



***Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Mhe. Muhammed Khamis Hamad, akishiriki zoezi la kupiga kura katika kituo cha kupigia cha Skuli ya Sekondari ya Kisauni, Jimbo la Dimani, Shehia ya Kisauni, Wilaya ya Magharibi B, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja wakati wa  Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 29, 2025.***

## Uchaguzi Mkuu 2025




*Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Ofisi ya Zanzibar, Mhe. Khatibu Mwinyi Mwinyichande, akipiga kura katika kituo cha kupigia kura cha Skuli ya maandalizi Fumba, Shehia ya Fumba, jimbo la Dimani, Wilaya ya Magharibi B, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Oktoba 29, 2025.*

## Ziara ya Waziri



*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Juma Zuberi Homera (Mb) akisaini kitabu cha wageni mara baada ya kuwasili katika Ofisi za Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Makao Makuu Dodoma kwa lengo la Kujitambulisha Novemba 26, 2025 .*

## Ziara ya Waziri




*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt Juma Zuberi Homera (katikati) akiwa na Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Zainabu Katimba (wa Pili Kulia), Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) Mhe. Jaji Mathew Mwaimu (Mst) (wa Pili kushoto), Makamu Mwenyekiti THBUB Mhe. Mohamed Khamis Hamad ( wa kwanza Kushoto), Naibu Katibu Mkuu Wizra ya Katiba na Sheria Dkt Franklin Rwezimula pamoja na Menejimenti ya THBUB Mara baada ya kuwasili ka¬tika Ofisi za Taasisi hiyo Novemba 26, 2025.*

## Maadhimisho Siku ya Maadili



*Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) ofisi ya Zanzibar, Mhe. Khatibu Mwinyi Mwinyichande (katikati) aliposhiriki kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu Zanzibar, Desemba 15, 2025 katika ukumbi wa mikutano uliopo Dimani, Wilaya ya Magharibi B, Mkoa wa Mjini Magharibi ambako Mgeni rasmi alikua Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi (hayupo pichani) Kushoto ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu ya Zanzibar, Mhe. Saada Mkuya Salum na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Zanzibar (CAG), Dkt. Othman Abas Ali (wa kwanza kulia).*

## Maadhimisho Siku ya Maadili



***Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) ofisi ya Zanzibar, Mhe. Khatibu Mwinyi Mwinyichande (katikati) alipojumuika pamoja na hadhara iliyohudhuria kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu Zanzibar, wakitoa heshima kwa wimbo wa Taifa, Desemba 15, 2025 katika ukumbi wa mikutano uliopo Dimani, Wilaya ya Magharibi B, Mkoa wa Mjini Magharibi.***

## **Maonesho** Jumuiya ya Waislamu




***Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB), Mhe. Mathew P. M. Mwaimu (Jaji Mst) alipotembelea baadhi ya mabanda ya taasisizilizoshiriki katika maonesho yaliyoandaliwa na Ju¬muiya ya Waislam Ahmadiyya Jijini Dar es Salaam Septemba 27, 2025.***

**MAWASILIANO**

**Mtaa wa Nyerere,** Plot Na. 339/Kilimani

S.L.P 1049 DODOMA, Tanzania

Simu: +255 738 279744

Barua Pepe:

**www.chragg.go.tz**